KAULI YA MAELEZO YA CHANJO

# Chanjo ya COVID-19:
*Unachohitaji Kujua*

Many Vaccine Information Statements are available in Swahili and other languages. See www.immunize.org/vis

Kauli nyingi za taarifa ya chanjo zinapatikana katika Kiswahili na lugha nyinginezo. Angalia www.immunize.org/vis

## 1. Je, kwa nini uchanjwe?

**Chanjo ya COVID-19** inaweza kuzuia **ugonjwa wa COVID-19**. Chanjo inaweza kusaidia kupunguza makali ya ugonjwa wa COVID-19 ikiwa utakuwa mgonjwa.

COVID-19 husababishwa na virusi vya corona vinavyoitwa SARS-CoV-2 ambavyo husambaa kwa urahisi kutoka kwa mtu hadi mwengine. COVID-19 inaweza kusababisha ugonjwa mdogo hadi wa wastani unaodumu kwa siku chache tu, au ugonjwa mbaya unaohitaji kulazwa hospitalini, wagonjwa mahututi au kipumuaji cha kusaidia kupumua. COVID-19 inaweza kusababisha kifo pia.

Dalili za COVID-19 zinaweza kuonekana siku 2 hadi 14 baada ya kuambukizwa virusi. Mtu anaweza kuwa na dalili hafifu, wastani, au kali.

- Dalili zinazoweza kutokea ni pamoja na joto kali; baridi; kohozi; kushindwa kupumua au kupumua kwa shida; uchovu (unyonge); maumivu ya misuli au mwili; maumivu ya kichwa; kupoteza ladha au harufu mpya; vidonda vya koo; kufungana mapua au mafua; kichefuchefu; kutapika; na kuhara.
- Dalili mbaya zaidi zinaweza kujumuisha kupumua kwa shida, maumivu ya mara kwa mara au shinikizo kwenye kifua, kuchanganyikiwa kupya, kutoweza kuamka au kukaa macho, au ngozi hafifu, kijivu au samawati, midomo au kucha, (kutegemea na rangi ya ngozi).

Watu wazima zaidi na watu wa umri wowote walio na hali fulani za kiafya (kama vile ugonjwa wa moyo au mapafu au kisukari) wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuugua COVID-19.

Baada ya ugonjwa wa COVID-19, watu wengine hupata COVID ya muda mrefu, hali sugu yenye dalili ambazo hudumu miezi 3 au zaidi. Dalili za COVID ya muda mrefu zinaweza kuwa kuimarika, kuwa mbaya zaidi, au kubaki vile vile.

Watu ambao wamepata chanjo zote za COVID-19 kufikia sasa wana hatari ndogo ya ugonjwa mbaya, kulazwa hospitalini na vifo kutoka kwa COVID-19 kuliko watu ambao hawajapata chanjo zote hizi kufikia sasa. Chanjo ya COVID-19 ndiyo njia bora ya kuzuia COVID ya muda mrefu.

Kupata chanjo ya COVID-19 husaidia mwili kujifunza jinsi gani kujikinga na ugonjwa huo na kupunguza hatari ya kugonjeka vibaya na matatizo. Zaidi ya hayo, chanjo za COVID-19 zinaweza kutoa ulinzi zaidi kwa watu ambao tayari wamekuwa na COVID-19, ikiwa ni pamoja na ulinzi dhidi ya kulazwa hospitalini ikiwa wataambukizwa tena na COVID-19.

## 2. Chanjo ya COVID-19

Upokeaji wa chanjo zote za kufikia sasa za COVID-19 za 2024–2025 unapendekezwa kwa kila mtu aliye na umri wa miezi 6 na zaidi. Hii inajumuisha watu ambao ni wajawazito, wanaonyonyesha, au wanaojaribu kupata mimba sasa, au ambao wanaweza kupata mimba katika siku zijazo.

Chanjo za COVID-19 za 2024–2025 kwa watoto wachanga na watoto wadogo miezi 6 hadi miaka 11 inapatikana kwenye Uidhinishaji wa Matumizi ya Dharura kutoka U. S. Food and Drug Administration (FDA). Tafadhali rejelea Majedwali ya Ukweli kwa Wapokezi na Watoa Utunzaji kwa maelezo zaidi.

Kwa watu walio na umri wa miaka 12 na zaidi, chanjo za COVID-19 za 2024–2025, zinazotengenezwa na ModernaTX, Inc. au Pfizer, Inc., zimeidhinishwa na FDA.

Chanjo ya Novavax COVID-19 Adjuvanted (2024–2025 Formula) inapatikana chini ya Uidhinishaji wa Matumizi ya Dharura kutoka kwa FDA kwa watu walio na umri wa miaka 12 na zaidi. Tafadhali rejelea Majedwali ya Ukweli kwa Wapokezi na Watoa Utunzaji kwa maelezo zaidi.

- **Kila mtu aliye na umri wa miezi 6 na zaidi** anapendekezwa kupokea chanjo inayolingana na umri iliyoidhinishwa na FDA au iliyoidhinishwa iliyosasishwa ya 2024–2025 ya COVID-19.
- **Watu fulani, kama wale walio na hali ya kiafya au wanaotumia dawa zinazoathiri mfumo wa kinga** wanaweza kuhitaji dozi za ziada za chanjo ya COVID-19. Mtoa huduma wako wa afya anaweza kukushauri.

CDC U.S. CENTERS FOR DISEASE CONTROL AND PREVENTION

## 3. Zungumza na mtoa huduma za afya wako

Mwambie mtoa huduma ya chanjo wako ikiwa mtu anayepokea chanjo:

- Amekuwa na **mmenyuko wa mzio baada ya dozi ya awali ya chanjo ya COVID-19**, au ikiwa ana mizio yoyote **mibaya, inayohatarisha maisha**
- Amekuwa na **myocarditis** (kuvimba kwa misuli ya moyo) au **pericarditis** (kuvimba kwa sehemu ya nje ya moyo)
- Amekuwa na **ugonjwa wa uvimbe wa mifumo mingi** (inayoitwa MIS-C kwa watoto na MIS-A kwa watu wazima)

Katika baadhi ya visa, mtoa huduma wako wa afya anaweza kuamua kuahirisha chanjo ya COVID-19 hadi ziara ya hapo baadaye.

Watu walio na magonjwa madogo, kama vile mafua, wanaweza kuchanjwa. Watu ambao ni wagonjwa kwa wastani au wagonjwa vibaya ikiwa ni pamoja na COVID-19, wanapaswa kwa kawaida kungojea hadi wapone.

Chanjo ya COVID-19 inaweza kutolewa wakati mmoja na chanjo nyingine.

## 4. Hatari za mmenyuko unaotokana na chanjo

- Maumivu, uvimbe, au wekundu unapodungwa sindano, joto kali, uchovu (utakalifu), maumivu ya kichwa, baridi, maumivu ya misuli, maumivu ya viungo, kichefuchefu, kutapika na kuvimba kwa nodi za limfu kunaweza kutokea baada ya chanjo ya COVID-19.
- Myocarditis (kuvimba kwa misuli ya moyo) au pericarditis (kuvimba kwa sehemu ya nje ya moyo) vimeonekana mara chache baada ya chanjo ya COVID-19. Hatari hizi zimeonekana mara nyingi kwa vijana wa kiume na wachanga. Uwezekano wa hatari hii kutokea ni wa chini.

Watu huzirai wakati mwingine baada ya taratibu za kimatibabu, ikiwemo kuchanjwa. Mwambie mtoa huduma wako ikiwa unahisi kizunguzungu au mabadiliko katika kuona kwako au kuhisi milio masikioni.

Kama ilivyo na dawa yoyote ile, kuna uwezekano mdogo sana kwa chanjo kusababisha mmenyuko mkali wa mzio, majeraha mengine mabaya, au kifo.

V-safe ni mfumo wa kufuatilia usalama ambao hukuwezesha kuielezea CDC jinsi wewe, au mtegemezi wako, unajihisi baada ya kupokea chanjo ya COVID-19. Unaweza kupata maelezo na kujiandikisha katika V-Safe katika [vsafe.cdc.gov](vsafe.cdc.gov).

Swahili translation provided by Immunize.org

## 5. Je, itakuwaje ikiwa kuna tatizo mbaya sana?

Mmenyuko wa mzio unaweza kutokea baada ya mtu aliyechanjwa kuondoka kwenye kliniki. Ikiwa utaona dalili za mmenyuko mkali wa mzio (mabaka, kuvimba uso na koo, matatizo ya kupumua, moyo kupiga haraka, kizunguzungu, au udhaifu), piga simu **9-1-1** na mtu huyo apelekwe kwenye hospitali iliyo karibu.

Tafuta matibabu mara moja ikiwa mtu aliyepokea chanjo anapata maumivu ya kifua, kushindwa kupumua, au hisia za kuwa na mapigo ya moyo yanayodunda kwa kasi, kutetemeka au kudunda kwa moyo baada ya chanjo ya COVID-19. Hizi zinaweza kuwa dalili za myocarditis au pericarditis.

Kuhusu ishara zingine ambazo zinakupatia wasiwasi, pigia simu mtoa huduma wa afya wako.

Athari mbaya zinapasa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (Vaccine Adverse Event Reporting System, VAERS). Mtoa huduma wako wa afya kwa kawaida ataandikisha ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe. Tembelea tovuti ya VAERS katika [www.vaers.hhs.gov](www.vaers.hhs.gov) au piga simu **1-800-822-7967**. *VAERS ni ya kuripoti mizio pekee, na wahudumu wa VAERS hawapeani ushauri wa kimatibabu.*

## 6. Mpango wa Hatua za Ufidiaji wa Majeraha (Countermeasures Injury Compensation Program)

Mpango wa Hatua za Ufidiaji wa Majeraha (CICP) ni mpango wa serikali kuu ambao unaweza kusaidia kulipia gharama za uuguzi wa kimatibabu na gharama nyingine mahususi za watu fulani ambao wamejeruhiwa vibaya sana na dawa fulani au chanjo, ikiwemo hii chanjo. Kwa jumla, madai yanafaa kuwasilishwa kwa CICP ndani ya mwaka mmoja (1) kutoka tarehe ya kupokea chanjo. Ili kujifunza zaidi kuhusu programu hii, tembelea tovuti ya programu katika [www.hrsa.gov/cicp](www.hrsa.gov/cicp), u piga simu **1-855-266-2427**.

## 7. Je, ninawezaje kujifunza mengi zaidi?

- Muulize mtoa huduma wako wa afya.
- Piga simu kwa idara ya afya ya eneo au ya jimbo lako.
- Tembelea tovuti ya Usimamizi wa Chakula na Dawa (FDA) kwa Maelekezo ya Ukweli kuhusu COVID-19, vipengee vya kifurushi na maelezo ya ziada katika [https://www.fda.gov/emergency-preparedness-and-response/coronavirus-disease-2019-covid-19/covid-19-vaccines](https://www.fda.gov/emergency-preparedness-and-response/coronavirus-disease-2019-covid-19/covid-19-vaccines).
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (Centers for Disease Control na Prevention - CDC):
  - Piga simu **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC ya chanjo za COVID-19 kwa [www.cdc.gov/covid/vaccines/index.html](www.cdc.gov/covid/vaccines/index.html).